# PDPC FARAGHA NEWSLETTER

ISSN 0000-0000 Na. 0001 JULAI-DESEMBA 2024


## FARAGHA ZILINDWE KWENYE UCHUMI WA KIDIGITALI

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) ***Dkt. Emmanuel Mkilia*** amesisitiza kulindwa kwa faragha za watu hasa kwa kipindi hiki ambacho Tanzania na Dunia zinajikita katika Uchumi wa kidigitali. >> **UK.6**

## Tanzania yapiga hatua Usalama wa Taarifa Binafsi

"Taasisi mbalimbali nchini Tanzania zimeanza kushirikiana kupitia Mfumo wa Jamii Exchange unaowezesha kubadilishana Taarifa". Amesema ***Dkt. Mkilia*** >> **UK.9**

## Ulinzi wa Taarifa Binafsi ni jukumu la kila mmoja wetu

Naibu Waziri wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari,**Mhandisi Maryprisca Mahundi** ameitaka jamii kushirikiana na viongozi wa kisekta,watetezi wa Faragha na uhuru wa Raia ili kuwa na Taifa linaloheshimu Faragha na kuwalinda watumiaji wa Taarifa kwenye uchumi unaendeshwa na Taarifa. UK. 17



**Dkt. Emmanuel Mkilia**
**Mkurugenzi Mkuu - PDPC**

Makala Maalumu - Chimbuko la Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Tanzania >> UK.14

# YALIYOMO


* TUMIENI TEKNOLOJIA VIZURI KULINDA TAARIFA BINAFSI - UK.5
* FARAGHA ZILINDWE, KWENYE UCHUMI WA KIDIGITALI - UK. 6
* TANZANIA YAPIGA HATUA USALAMA WA TAARIFA BINAFSI - UK.9
* TUZINGATIE KANUNI ZA DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI - UK.11
* JAMII YASHAURIWA KULINDA TAARIFA BINAFSI - UK.13
* CHIMBUKO LA SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI TANZANIA - UK.14
* MAAFISA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI WAJENGEWE UWEZO NA TAASISI ZAO - UK.18
* HABARI PICHA - UK.22
* TAARIFA BINAFSI NI NYENZO MUHIMU KWENYE UCHUMI WA KIDIJITALI - UK.26
* ZINGATIENI HAKI YA FARAGHA, MNAPOSANIFU MIFUMO YA TEHAMA - UK.29


**SCAN HAPA KUISAJILI TAASISI/OFISI YAKO KWENYE MFUMO WA USAJILI NA UZINGATIAJI (RCMIS) WA TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI**





## SALAMU KUTOKA KWA MKURUGENZI MKUU WA TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

**Ndugu Msomaji,**

Ni furaha kubwa kwangu kukusalimu kupitia toleo hili la kwanza la jarida la "Ulinzi wa Taarifa Binafsi". Jarida hili ni sehemu muhimu ya mkakati wa Tume kuhakikisha kuwa jamii inapata elimu sahihi kuhusu masuala ya ulinzi wa taarifa binafsi, haki ya faragha, na wajibu wa wadau katika kutekeleza Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Na. 11 ya 2022.

Katika dunia ya sasa yenye maendeleo makubwa ya kidijitali, elimu kwa umma kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi ni nyenzo muhimu katika kuhakikisha usalama wa taarifa za watu. Wananchi wanapaswa kufahamu jinsi ya kulinda taarifa zao, madhara yanayoweza kujitokeza endapo zitadhibitiwa vibaya, na hatua zinazopaswa kuchukuliwa pale ambapo haki yao ya faragha inavunjwa. Jarida hili litakuwa chombo cha kuhamasisha, kuelimisha na kuhimiza uwajibikaji katika usimamizi wa taarifa binafsi.

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha kuwa ulinzi wa taarifa binafsi unazingatiwa katika sekta zote. Kupitia jarida hili, tutakuwa tukitoa taarifa kuhusu matukio mbalimbali, mafanikio ya utekelezaji wa sheria, na changamoto zinazojitokeza ili kujenga jamii yenye uelewa mpana wa haki na wajibu wao katika kulinda taarifa binafsi.

Natoa rai kwa kila mmoja kushiriki kikamilifu katika safari hii ya kulinda taarifa binafsi kwa manufaa ya taifa letu. Tunakaribisha maoni, ushauri, na michango yenu katika kuboresha jarida hili na kuhakikisha linakuwa na mchango chanya kwa jamii.

Asanteni kwa kuunga mkono juhudi za ulinzi wa taarifa binafsi nchini.

**Dkt. Emmanuel Lameck Mkilia**
Mkurugenzi Mkuu



# BODI YA WAHARIRI



**Mwenyekiti**
**Dkt. Emmanuel Mkilia**



**Mjumbe**
**Mhandisi Stephen Wangwe**



**Mjumbe**
**Wakili Humphrey Mtuy**



**Mjumbe**
**Dkt. Noe Nnko**



**Mjumbe**
**Rehema Abdallah**



**Mhariri Mkuu**
**Innocent Mungy**



# TAHARIRI YA MHARIRI



Karibu kwenye toleo la kwanza la jarida la "Ulinzi wa Taarifa Binafsi", jarida rasmi la Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC). Jarida hili limeanzishwa kwa dhamira ya kuwa chanzo cha taarifa sahihi, elimu, na mwongozo kwa umma kuhusu dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi, wajibu wa wadau mbalimbali, na hatua zinazochukuliwa kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Na. 11 ya 2022 pamoja na Kanuni zake.

Katika dunia ya sasa, ambapo matumizi ya teknolojia ya kidijitali yanaongezeka kwa kasi, suala la ulinzi wa taarifa binafsi limekuwa muhimu kuliko wakati wowote ule. Taarifa binafsi zina thamani kubwa na zinapaswa kulindwa kwa mujibu wa sheria ili kuzuia matumizi mabaya, ukiukwaji wa faragha, na madhara yanayoweza kusababishwa na upatikanaji usio halali wa taarifa hizo. Ndiyo maana Tume imejizatiti kuhakikisha kuwa sheria inatekelezwa kwa ufanisi, huku tukitoa elimu kwa umma na wadau mbalimbali ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu haki na wajibu wao.

Jarida hili litatolewa kila robo mwaka likihusisha habari, tafiti, na matukio muhimu yanayohusiana na ulinzi wa taarifa binafsi ndani ya kipindi husika. Katika toleo hili la kwanza, tutakuletea muhtasari wa hatua zilizochukuliwa tangu kuanzishwa kwa Tume, mafanikio yaliyopatikana, changamoto zilizojitokeza, na mwelekeo wa siku zijazo. Vilevile, tutakuwa na makala maalum zinazofafanua dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi, hadithi za mafanikio, na maoni kutoka kwa wataalamu wa sekta mbalimbali kuhusu umuhimu wa kulinda taarifa za watu.

Tume inaamini kuwa kila mtu ana wajibu wa kushiriki katika kulinda taarifa binafsi, iwe ni taasisi za umma, sekta binafsi, au wananchi kwa ujumla. Hivyo basi, tunakukaribisha usome na kushiriki mawazo yako nasi ili kwa pamoja tujenge jamii inayotambua thamani ya faragha na haki ya ulinzi wa taarifa binafsi.

Tunaahidi kuendelea kuwaletea maudhui yenye tija, maarifa, na mwongozo wa kitaalamu ili kuhakikisha kuwa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi inatekelezwa ipasavyo kwa manufaa ya wote. Endelea kufuatilia jarida hili kwa habari na uchambuzi wa kina kuhusu maendeleo ya ulinzi wa taarifa binafsi nchini Tanzania.

**Innocent P. M. Mungy**
**Mhariri Mkuu**
**Jarida la "Ulinzi wa Taarifa Binafsi"**

## TUMIENI TEKNOLOJIA VIZURI KULINDA TAARIFA BINAFSI

Taasisi nchini zimetakiwa kuzingatia matumizi ya teknolojia zinazowezesha kulinda taarifa ili kuhakikisha hakuna uvunjifu wa Sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi nchini.

Hayo yalisemwa kwenye warsha ya ulinzi wa taarifa iliyofanyika jijini Dar es Salaam kwa lengo la kujadili teknolojia zinazoweza kusaidia kuimarisha ulinzi wa taarifa binafsi kwenye taasisi nchini Tanzania wakati taasisi hizo zikianza kutekeleza sheria hiyo ya ulinzi wa taarifa binafsi ya mwaka 2022.

Akizungumza kwenye warsha hiyo, Mkurugenzi wa Kitengo cha Tafiti za Ulinzi wa Taarifa na Teknolojia kutoka Tume ya Ulinzi wa taarifa binafsi (PDPC), Dkt. Noe Nnko amezitaka taasisi za umma na binafsi nchini kuhakikisha zinazingatia sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi kwa kutumia teknolojia vizuri na kulinda taarifa hizo.

"Taasisi zote za umma na binafsi lazima zihakikishe zimejisajili na kupata cheti cha PDPC kabla ya Disemba, 2024 ili kutii maagizo ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuheshimu sheria kwani kutokufanya hivyo ni kosa" Alisema Dkt. Nnko

# Faragha zilindwe kwenye Uchumi wa kidigitali

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Dkt. Emmanuel Mkilia amesisitiza kulindwa kwa faragha za watu hasa kwa kipindi hiki ambacho Tanzania na dunia zinajikita katika Uchumi wa kidigitali.

Hayo yalielezwa na Dkt. Mkilia wakati akifanya mahojiano na kituo cha televisheni cha TBC kwenye kipindi cha Mizani ikiwa ni moja ya njia ya kutoa elimu kwa umma ili dhana nzima ya Ulinzi wa taarifa binafsi iweze kueleweka kwa jamii wakiwemo wahusika wa taarifa, wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi.

"Tumehakikisha Tume ina uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kwa sasa tunatoa elimu kwa umma ili kuleta uelewa wa pamoja kwa mtoa taarifa, wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi, kusimamia sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi kwa kusajili wakusanyaji na wachakataji wa taarifa hizo na kuwapatia vyeti vinavyoonyesha kuwa wapo tayari kufuata sheria hiyo". Alisema Dkt. Mkilia

"Kwa sasa hivi kuna huduma nyingi zinatolewa kwa njia ya kidigitali, mteja mkubwa ni huyu muhusika wa taarifa tunayemzungumzia na ili kupata huduma hizo analazimika kutoa taarifa zake binafsi hivyo ni muhimu kujihakikishia kuwa taarifa hizo zinatumika inavyotakiwa na faragha yake inalindwa ili kujenga Tanzania inayojali utu, haki za binadamu na faragha za watu tunavyoendelea kujikita katika Uchumi wa kidigitali" .

Pia Dkt. Mkilia amezitaka taasisi zote za Serikali na binafsi kujisajili na kuhakikisha wanapata cheti cha usajili cha PDPC ili kujenga imani na kupata fursa ya kutekeleza majukumu yao ndani na nje ya mipaka ya nchi kwa kuwa watakuwa wanazingatia sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi katika utekelezaji wa majukumu yao.



**Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Dkt. Emmanuel Mkilia akiwa kwenye Studio za TBC 1, jijini DSM**

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) ni tume huru liyoundwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 16 (1) na (2) inayotoa haki ya faragha kwa kila mwananchi na kuelekeza kuundwa kwa chombo cha kusimamia ulinzi wa faragha hizo na ilizinduliwa rasmi tarehe 3 Aprili 2024 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

# TPPA SAIDIENI TAASISI KUTEKELEZA PDPA

Bw. Innocent Mungy, Mkuu wa Uhusiano na Mawasiliano, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) amewataka wanachama wa Chama cha Wataalamu wa Faragha Tanzania (TPPA) kusaidia taasisi za umma na binafsi kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Na 11 ya mwaka 2022.

Akizungumza na wanachama hao kwenye mkutano wa TPPA uliofanyika Dar es Salaam kwa lengo la kukutana na kubadilishana ujuzi wa kitaaluma, Bw. Mungy amewataka wataalamu hao kushiriki katika jitihada za Serikali za kutoa elimu kwa umma na kuzisaidia taasisi za umma na binafsi kutekeleza sheria hii.

Aida Bw. Mungy aliwashukuru wanachama wa TPPA kwa kuwa mstari wa mbele katika kuelimisha umma na kutambua mchango wao katika kusaidia utekelezaji wa sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi, na aliwakaribisha kufanya ushirikiano zaidi katika maeneo mengine ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.



# ELIMU DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI YAPIGIWA CHAPUO



Ili kuimarisha Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini, wakuu wa Taasisi zinazokusanya na kuchakata Taarifa binafsi wameshauriwa kuhakikisha watumishi wote kwenye taasisi zao wanapata uelewa kuhusu Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Wito huo ulitolewa Novemba 18,2024 jijini DSM na Mkurugenzi wa Usajili na Uzingatiaji - Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Mhandisi Stephen Wangwe wakati akitoa mafunzo maalumu ya Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa watumishi wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ambapo alisema ili kupata matokeo chanya ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwenye Taasisi ni vema watumishi wote wakapata elimu kuhusu dhana hiyo.

" Ni vizuri kwenye Taasisi watumishi wote mpaka wale wa ngazi ya chini kabisa wakapata elimu kuhusu dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ili kuhakikisha kila mtu analinda Taarifa kwenye Taasisi" amesema Mhandisi Wangwe.

Kwa upande wake Dkt. Noe Nnko, Mkurugenzi wa Tafiti za Taarifa Binafsi na Teknolojia - PDPC akatumia fursa hiyo kuzikumbusha Taasisi kutokuchakata taarifa kwa siri bali watumie sera ya faragha kama sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi inavyotaka.

Wakati huo huo Bw. Innocent Mungy Mkuu wa Uhusiano na Mawasiliano - PDPC alisisitiza elimu ya dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kuwa endelevu kwa Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPO) wa kila taasisi itakayojisajili PDPC ili kuhakikisha Taarifa Binafsi za watu zilizopo kwenye taasisi zao hazitumiki vibaya.

Mafunzo hayo ya siku moja kwa watumishi wa NSSF ni sehemu ya mpango mkakati wa PDPC wa kuendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu Utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Na. 11 ya Mwaka 2024.

> Ni vizuri kwenye Taasisi watumishi wote mpaka wale wa ngazi ya chini kabisa wakapata elimu kuhusu dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi
>
> **Mhandisi Wangwe**



Baadhi ya Watumishi wa NSSF wakifatilia Mada ya Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi iliyokua inatolewa na Wataalamu kutoka PDPC



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia (Kushoto) Akimpokea Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Marryprisca Mahundi alipotembelea Ofisi za PDPC - Dodoma,

## PDPC YAPONGEZWA KWA KUFANYA KAZI KWA WELEDI

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) imepongezwa kwa kufanya kazi kwa weledi na Ushirikiano.

Pongezi hizo zimetolewa jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, **Mhe. Mhandisi Maryprisca Mahundi (Mb)**, wakati wa Ziara yake ya kikazi katika ofisi za Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi zilizopo Jengo la UCSAF - Dodoma ambapo alisema PDPC ni Taasisi changa ila inafanya kazi kwa weledi na ushirikiano.

Aidha Mhandisi Mahundi aliwataka watumishi wa PDPC kuendelea kufanya kazi kwa dhati na kuongeza ushirikiano ili kuleta matokeo chanya kwenye sekta ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini.

"Tume hii ni moja ya vipaumbele vya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan** hivyo tunapaswa kumsaidia kutimiza maono yake" Alisema Mhandisi Mahundi

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Dkt. Emmanuel Mkilia aliweka bayana baadhi ya majukumu ya PDPC ikiwa ni pamoja na Kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, kusajili Taasisi zote zinazokusanya na kuchakata Taarifa, Kufanya Tafiti na kufatilia Maendeleo ya Teknolojia yanayoathiri Usalama wa Taarifa Binafsi, Kupokea, kuchunguza na kushughulikia Malalamiko yanayohusiana na ukiukwaji wa haki za Faragha.



## TANZANIA YAPIGA HATUA USALAMA WA TAARIFA BINAFSI

Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimefanya Mkutano kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi wenye lengo la kubadilishana ujuzi wa Ulinzi wa Taarifa na uthibitishaji wa mfumo wa sera ya usimamiaji wa Taarifa.

Mkutano huo ulifanyika katika hoteli ya Radisson Parking Inn jijini Kigali, nchini Rwanda.

Pia Dkt Mkilia alisisitiza umuhimu wa kuwa na miundombinu ya kuaminika katika kushirikishana taarifa kati ya nchi na nchi.

"Ni lazima kuwe na uaminifu katika miundombinu ili kuruhusu utumaji wa Taarifa kwa usawa na ubora unaolingana, hivyo kuimarisha ushirikiano katika Ulinzi wa Taarifa Binafsi." Alisema Dkt. Mkilia




Katika mkutano huo, Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia alieleza kuwa Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuhakikisha kuna usalama wa taarifa binafsi kwa kutunga sheria inayohusiana na Ulinzi wa Taarifa Binafsi, kuanzishwa kwa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi pamoja na kuwepo kwa Kituo cha Data cha Taifa.

Mkutano huo wa siku tatu (3) uliofanyika jijini Kigali ulianza tarehe 16 na ulimalizika tarehe 18/10/2024 ambapo ulishirikisha nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na Tume za Ulinzi wa Taarifa Binafsi zilizopo kwenye nchi hizo. Kwa upande wa Tanzania, PDPC iliwakilishwa na Mkurugenzi Mkuu wa PDPC Dkt Emmanuel Mkilia, Mkurugenzi wa Utafiti na Maendeleo ya Teknolojia PDPC Dkt. Noe Nko.

# HAKIKISHENI TAASISI ZENU ZINATEKELEZA SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Lameck Mkilia, amewataka Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi kuhakikisha Taasisi zao zinatekeleza Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa weledi.

Dkt. Mkilia ameyasema hayo Desemba 18, 2024 wakati wa hafla ya kufunga warsha ya uhamasishaji wa ulinzi wa Taarifa Binafsi iliyofanyika jijini Dar es Salaam. Warsha hiyo iliyohusisha maafisa wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPOs) imeweka msingi wa uelewa na utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini.

Katika hotuba yake, Dkt. Mkilia alisisitiza kuwa warsha hiyo ni hatua muhimu kuelekea kuimarisha Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini, akiwataka washiriki kuchukua hatua za msingi ili kutekeleza Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

“Nitoe wito kwenu kuandaa mipango ya utekelezaji wa majukumu yenu kwa kila robo mwaka na kuhakikisha Taasisi zenu zinafuata matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi” amesema Dkt. Mkilia

Aidha Dkt. Mkilia amewahakikishia maafisa hao kuwa PDPC itaendelea kutoa msaada na mwongozo kuhakikisha Tanzania inakuwa mfano wa kuigwa Duniani katika utekelezaji wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

"Kwa pamoja, tushirikiane kuhakikisha Ulinzi wa Taarifa Binafsi unakuwa nguzo kuu ya mageuzi ya kidijitali nchini Tanzania," alihitimisha Dkt. Mkilia.









Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi(PDPC), **Balozi. Rajabu Adadi** (kushoto) akiwa na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), **Mhandisi Zena Ahmed Said** wakati wa hafla ya ufunguzi wa Semina ya kujenga uelewa kuhusu Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa Makatibu wakuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliyofanyika Novemba 29, 2024 Visiwani Zanzibar.

# TUZINGATIE KANUNI ZA DHANA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, ni dhana muhimu wakati huu wa mabadiliko ya kidijitali duniani hivyo ili kuendana na kasi ya maendeleo ya teknolojia duniani, viongozi wa kada mbalimbali nchini wameshauriwa kuzingatia kanuni za dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kila wanapokua kwenye majukumu yao ya kila siku ili kuleta matokeo chanya kwenye sekta ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

Hayo yameelezwa Novemba 29, 2024 visiwani Zanzibar na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Dkt. Emmanuel Mkilia wakati wa hafla ya Ufunguzi wa semina kuhusu Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa Makatibu Wakuu wa SMZ ambapo amesema kama msingi wa Demokrasia ni wajibu wa kila kiongozi kuhakikisha haki ya Faragha inazingatiwa katika majukumu yao ya kikazi. *Inaendelea UK.12*

*Inatoka UK.11*

"Kama msingi wa demokrasia katika nchi yetu, pia Ulinzi wa Taarifa Binafsi umebainishwa na kuahidiwa pia katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 kipengele cha 61 (b). Kwa ajili hiyo basi, ni wajibu na jukumu letu, kama viongozi na watumishi wa umma, kuhakikisha kuwa haki hii inaheshimiwa katika mamlaka zetu." Amesema Dkt. Mkilia

Aidha ACP Mkilia akawataka Makatibu Wakuu hao kuitumia Fursa hii ya Mafunzo kujadiliana kwa kina kuhusu Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

" Tunapokusanyika hapa leo, hii ni fursa ya kujifunza na kutathimini umuhimu wa dhana nzima ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi katika nchi yetu na maisha ya wananchi lakini pia Ulinzi na Usalama wa Taarifa za Taifa letu katika enzi ambapo Taarifa zetu zinakusanywa na kuchakatwa kwa urahisi." Alisema Dkt. Mkilia.

PDPC kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi – Zanzibar waliandaa Semina hii ya siku moja kwa Makatibu Wakuu wa SMZ kwa lengo la kuwajengea uwezo kuhusu Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Nchini.



*Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia na Bi. Hawwah Ibrahim Mbaye, Naibu Katibu Mkuu (Mawasiliano) katika Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi - Zanzibar wakifatilia mada kwenye Semina kuhusu Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi iliyotolewa kwa Makatibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliyofanyika Visiwani Zanzibar Novemba 29,2024.*



*Bi. Hawwah Ibrahim Mbaye, Naibu Katibu Mkuu (Mawasiliano), Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi - Zanzibar akiwa na Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Bi. Fatuma Mohammed Ally kwenye Semina kuhusu Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi iliyotolewa kwa Makatibu Wakuu - SMZ*



*Bi. Rehema Abdalla, Mkurugenzi wa PDPC Zanzibar akizungumza na Makatibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwenye Hafla ya Ufunguzi wa Semina ya Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi iliyoandaliwa na PDPC ili kujenga uelewa wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa Viongozi hoa wa Visiwani Zanzibar*



*Bw.Hamid Haji Machano, Mjumbe wa Bodi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi akifatilia mada kwenye Semina kuhusu Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi iliyotolewa kwa Makatibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliyofanyika Visiwani Zanzibar Novemba 29,2024.*



# JAMII YASHAURIWA KULINDA TAARIFA BINAFSI

Katika hatua ya kuhakikisha Ulinzi wa faragha za wananchi unazingatiwa kwa mujibu wa Sheria nchini.

Jamii yashauriwa kulinda Taarifa zao kwa kutokuzitoa kwa taasisi ambazo hazijasajiliwa na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC).

Wito huo umetolewa Jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa Usajili na Uzingatiaji – PDPC, Mhandisi Stephen Wangwe wakati akifanya mahojiano na kituo cha redio cha Crown FM kupitia kipindi cha Kasri la Kikeke ambapo amesema kwa sasa PDPC wanasajili na kutoa vyeti kwa Taasisi zote zinazochakata na kukusanya Taarifa nchini hivyo kabla hujatoa Taarifa zako hakikisha kama hiyo Taasisi imesajiliwa.

"Kabla ya kutoa Taarifa zako kwa Taasisi yoyote nchini hakikisha kama wamesajiliwa na kupata cheti cha PDPC, hii itawezesha PDPC kusimamia Ulinzi wa Taarifa za watu na faragha zao."
Alisema Mhandisi Wangwe

Aidha Mhandisi Wangwe amesema PDPC wanatarajia kuandaa kanzi data (database) ambayo itaonesha ni Taasisi zipi zimesajiliwa na kupata vyeti ili wananchi wawe huru kutoa Taarifa zao pale zinapohitajika.

Katika hatua nyingine Mhandisi Wangwe akatoa wito kwa Wadau wa Maendeleo hasa vyombo vya habari kushirikiana na PDPC kutoa elimu katika jamii kuhusu dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi

" Tume tunashirikiana na wadau mbalimbali na hapa pia nitoe wito kwa hizi media groups na wengine wote wanaofanya kazi za uelimishaji waweze kushirikiana nasi kufikisha hii elimu kwa jamii,"

MAKALA MAALUMU

# Chimbuko la Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Tanzania (PDPA)




Machache yameandikwa kuhusu Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Tanzania, Sura ya 44 ya Sheria za Nchi (PDPA), bila shaka hayajaandikwa si kwasababu hayapo la hasha bali ni kutokana na ugeni au upya wa Sheria hii.

Makala hii imeandaliwa kwa lengo la kukupa elimu ya kina kuhusu Sheria hiyo na itaweka bayana kwanini Sheria hii ni muhimu kwa maendeleo ya Taifa na jamii kwa ujumla ambapo itaangazia faida na umuhimu wa Sheria yenyewe pamoja na chimbuko lake.

Katika kuyaangazia hayo kwanza nianze kwa kukujengea uelewa kuhusu maana ya Taarifa Binafsi ambapo baadhi ya watu wanadhani Taarifa Binafsi ni siri zao au ni zile Taarifa ambazo hazifai kumshirikisha mtu yeyote yule. La hasha! Taarifa Binafsi ni zile Taarifa zinazo mtambulisha mtu au zinazoweza kufanya mtu akatambulika, mfano Jina lake, jinsia yake, dini yake, kabila lake, namba yake ya simu, barua pepe yake, makazi yake, picha yake, kundi lake la damu (DNA), namba yake ya kitambulisho, leseni ya udereva, pasi ya kusafiria, NIDA, n.k.

Hivyo basi Taarifa yoyote ambayo unaona inaweza kukutambulisha popote pale hiyo ni Taarifa yako Binafsi na unapaswa kuilinda kama mboni ya jicho lako kwakua ikitumika vibaya inaweza kukuletea madhara mbalimbali ikiwemo wizi na kuharibika kwa staha au hadhi/heshima au utu wako (Reputation, Status or Dignity).

**ULINZI WA TAARIFA BINAFSI NI NINI?**

Ulinzi wa Taarifa Binafsi, ni hatua zinazolenga kuzuia matumizi mabaya ya Taarifa Binafsi ili kulinda faragha ya mhusika wa Taarifa. Hatua hizo ni za .... kimkakati na za kiutaratibu zinazochukuliwa wakati wa Ukusanyaji na/au Uchakataji wa Taarifa. Pengine unajiuliza kwa nini ulinde Taarifa zako Binafsi. Ni hivi, zipo sababu nyingi za msingi za wewe kufanya hivyo ila kwa uchache unapaswa kulinda Taarifa zako Binafsi ili:-

* Kuzuia Matumizi Mabaya ya Taarifa zako.
* kujilinda dhidi ya uhalifu wa mtandao unaoweza kusababisha madhara kwa mhusika kiuchumi, kijamii/kisiasa na kiusalama.
*Kulinda staha, heshima na utu wako;
* Kulinda amani ya moyo (Peace of mind). na
* Kuimarisha Uaminifu na Uadilifu (Trust and Integrity).

**CHIMBUKO LA SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI**

Haki ya Faragha inayotokana na Azimio la Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Binadamu ni miongoni mwa sababu za msingi zilizopelekea kuanzishwa kwa Kanuni za Jumla za Ulinzi wa Tarifa Binafsi za Umoja wa Ulaya inayotambulika kama "General Data Protection Regulations (GDPR)" ambayo ni mfumo wa kisheria wa ulinzi wa taarifa binafsi mkubwa zaidi Duniani kwa kuwa unahusisha wananchi wote wa Umoja wa Ulaya bila kujali walipo. Aidha, sababu nyingine kubwa ya umuhimu wa mfumo wa kisheria wa ulinzi wa taarifa binafsi ni uimarishaji wa uchumi wa kidijitali.

Naam Wapwani wanasema Mcheza kwao hutunzwa na sasa tuangazie Chimbuko la Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Tanzania (PDPA) ambayo ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mwaka 2022 na kuanza kutekelezwa rasmi Mwaka 2023.



Chimbuko la kutunga Sheria hii ilikuwa ni kutokuwepo kwa Sheria mahsusi na Chombo cha kusimamia wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi kwa kuainisha misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi; uhitaji wa kuifanya anga ya mtandao kuwa salama kwa kuoanisha na miongozo ya Kikanda na Kimataifa; kutekeleza maelekezo ya Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016; kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM (Chama tawala) ya mwaka 2020;

na umuhimu wa kuimarisha uchumi wa kidijitali pamoja na kuongeza uwekezaji kwenye Sekta ya TEHAMA nchini.

Kabla ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44 ya Sheria za Nchi, Tanzania ilikuwa na Sheria kadhaa zilizoshughulikia Ulinzi wa Taarifa na faragha za watu, ambapo baadhi ya Sheria hizo ni:

**Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai - 1985**
Sheria hii inatafsiri Mwenendo wa Mashauri ya Jinai ambapo kama mtu akikiuka Haki ya Faragha, inaeleza hatua za kufata katika kushughulikia Shauri hilo.

**Sheria ya Kuzuia Ugaidi 2002**
Sheria hii inaruhusu Taarifa Binafsi za Shahidi kutokuwekwa Hadharani yaani kufichwa ili kulinda haki yake ya Faragha na Usalama.

**Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha - 2006**
Sheria hii inazuia wafanyakazi wa Benki kutoa Taarifa Binafsi za Wateja wao kwa Mtu au Taasisi Yoyote.

**Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta - 2010 (EPOCA)**
Sheria hii inasimamia mawasiliano ya kielektroniki, mawasiliano ya simu na posta nchini Tanzania ambapo kupitia kifungu cha 98 cha Sheria hii wafanyakazi wa Ofisi za Mawasiliano ya Simu, Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta hawaruhusiwi kutoa Taarifa binafsi za Mteja kwa Mtu au Taasisi yoyote.

**Sheria ya Makosa ya Mtandao - 2015:** Sheria hii inaweka makosa yanayohusiana na ukiukaji wa faragha dhidi ya au kutumia mfumo wa kompyuta au Mtandao nchini ambapo kupitia kifungu cha 48 cha Sheria hii Mtu yoyote haruhisiwi kuweka (publishing) Taarifa Binafsi za Mtu Mtandaoni bila Ridhaa ya muhusika wa taarifa.

**FAIDA ZA SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI**
Kuna faida nyingi za Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi iwe kiuchumi, kisiasa au kijamii. Hapa tutaangazia faida hizi kwa Mtanzania mmoja mmoja bila kujali umri, cheo/nafasi wala jinsia na kwa Taifa kwa ujumla: -

1. **Kuifanya anga ya mtandao ya Tanzania kuwa salama kwa kuzingatia matakwa ya Mikataba na Miongozo ya Kikanda na Kimataifa kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi.**

2. **Kuongezeka kwa matumizi sahihi ya Taarifa Binafsi nchini.**

3. **Kuongezeka kwa amani na usalama nchini.**

4. **Kuongezeka kwa watumiaji wa huduma za mtandaoni kwa uhakika wa taarifa zao binafsi kuwa salama.**

5. **Kuongezeka kwa wawekezaji wa masuala ya teknolojia nchini na kuwapatia watanzania sifa na fursa ya kuwekeza nje ya nchi hususan kupitia mifumo ya TEHAMA.**

Naomba nitamatishe Makala hii kwa kukujuza kwamba Ulinzi wa Taarifa Binafsi unaanza na wewe mwenyewe hivyo linda Taarifa zako kwa kuhakikisha unazitoa pale zinapohitajika tu kulingana na huduma unayohitaji yaani kama unahitaji huduma ya kupewa cheti/vyeti basi toa Taarifa ambazo zinahusiana na wewe kupata hivyo vyeti , sio unahitaji Leseni ya Biashara wakulazimishe kutoa Taarifa ya Idadi ya Watoto ulionao hiyo sio sawa.



# ULINZI WA TAARIFA BINAFSI NI JUKUMU LA KILA MMOJA WETU




Naibu Waziri wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Maryprisca Mahundi ameitaka jamii kushirikiana na viongozi wa kisekta, watetezi wa Faragha na uhuru wa Raia ili kuwa na taifa linaloheshimu faragha na kuwalinda watumiaji wa Taarifa kwenye uchumi unaendeshwa na Taarifa.

Mhandisi Mahundi ametoa wito huo Novemba 15, 2024 jijini Arusha wakati akifunga kongamano la Anuai za kitaaluma lililoandaliwa na Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) kwa kushirikiana na Jumuiya ya Faragha Tanzania ambapo amesema ulinzi wa taarifa ni wa kila mtu na sio wa Serikali peke yake.

" Suala la Ulinzi wa Taarifa na la kila mmoja wetu na sio la Serikali peke yake kwani tunaishi katika enzi ambapo tyaarifa hutiririka katika tasnia, mipaka na mifumo ya ofisi kwa kasi kubwa hivyo tunatarajia kushiriki kwa pamoja sisi kama Serikali pamoja na wadau mbalimbali katika kufika malengo tulijowekea" alisema Mhandisi Mahundi.

Katika hatua nyingine Mhandisi Mahundi akatumia jukwaa hilo kukipongeza chama cha Wanasheria Tanganyika kwa kuandaa kongamano hili na kuwataka wanasheria nchini kuisadia Serikali katika kusimamia Sheria na utekelezaji wa sera mbalimbali za Ulinzi wa Taarifa nchini.

"Tunatarajia wanasheria mtatusaidia katika kusimamia sheria na sera mbalimbali zinazosimamia ulinzi wa taarifa ili kuimarisha hatari tunazokabiliana nazo kama vile ukiukwaji wa faragha na mashambulizi ya kimtandao" amesema Mhandisi Mahundi

Kongamano hili la siku tano (5) lililobebwa na kauli mbiu ya Ulinzi wa Taarifa katika Uchumi wa Sekta mbalimbali kujenga njia iliyo ya Faragha na Usalama limewakuwakutanisha pamoja wataalamu kutoka sekta mbalimbali nchini na kujadili kwa kina kuhusu dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi.



# MAAFISA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI WAJENGEWE UWEZO NA TAASISI ZAO

Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Bw. Mohammed Khamisi Abdulla ametoa wito kwa Taasisi na ofisi mbalimbali nchini kuwajengea uwezo maafisa ulinzi wa taarifa Binafsi - DPO's kwenye kada ya ulinzi wa Taarifa ili kuimarisha sekta hiyo.

Bw. Abdulla ametoa wito huo jijini Arusha wakati akifungua mafunzo ya siku nne ya Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi kutoka taasisi zilizo chini ya chama cha mabenki Tanzania - TBA na chama cha Watoa huduma za Mitandao ya simu Tanzania - TAMNOA ambapo amesema hakuna msamaha kwa kutokujua sheria hivyo maaafisa ulinzi wa Taarifa binafsi kwenye Taasisi.

"Tume itakua ikiratibu mafunzo haya kwa makundi mbalimbali leo ni kundi la mwanzo na mafunzo ya mwanzo hivyo nitoe Rai kwa Taasisi zote kuhakikisha maafisa wake wanajengewa uelewa na uwezo katika kutekeleza majukum ya Taasisi zao"

Aidha Bw. Abdulla akawataka maafisa hao kufanya kazi kwa weledi kwa kuzingatia Sera ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi " Mabenki na Kampuni za Simu zinafanya kazi katika mazingira yenye ushindani mkubwa na zinahitaji kuwa na Sera na taratibu bora za Ulinzi wa Taarifa binafsi za wateja wao ili kuhakikisha kuwa taarifa za wateja zinakuwa salama na zinalindwa vizuri".



Bw. Mohammed Khamisi Abdulla, Katibu Mkuu, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari,

Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi zaidi ya 90 kutoka Taasisi zilizo chini ya chama cha mabenki Tanzania - TBA na chama cha Watoa huduma za Mitandao ya simu Tanzania - TAMNOA wamejitokeza kushiriki mafunzo haya yanayoendeshwa na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC).

## TOA TAARIFA ZAKO KULINGANA NA HUDUMA UNAYOIHITAJI

Jamii yaaswa kuzingatia kutoa Taarifa zinazoendana na huduma wanayoihitaji kwa wakati huo ili kulinda Taarifa zao Binafsi.

Wito huo umetolewa jijini Mwanza na Bw. Innocent Mungy, Mkuu wa Uhusiano na Mawasiliano Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) wakati akifanya mahojiano maalumu kwenye kipindi cha Full Bando kinachorushwa hewani na kituo cha redio cha Afya FM ambapo alisema ili kulinda matumizi ya Taarifa zako Binafsi, unapaswa kuchuja na kuhakikisha unapoenda kupata huduma, unatoa Taarifa zinazoendana na huduma hiyo na si vinginevyo.

"Mfano unaenda kukata bima ya gari ila unaulizwa una wake wangapi una haki ya kuhoji, we unataka kujua wake zangu ni wangapi ili iweje? Akikwambia anataka kujua kama na yeye ana gari na anakata bima kampuni gani unamwambia hapana kama atahitaji bima atakuja yeye mwenyewe, mimi nimekuja kama mimi" alisema Bw. Mungy






Baadhi ya Viongozi wa PDPC, TBA na TAMNOA wakiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPO's) kutoka Taasisi mbalimbali nchini waliojotokeza kushiriki Mafunzo ya Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi yaliyofanyika Jijini Arusha (AICC), Julai 9 - 12, 2024

# TUSHIRIKIANE NA PDPC KUIMARISHA USALAMA WA TAARIFA BINAFSI NCHINI

Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) ameitaka Jamii kupitia Taasisi mbalimbali nchini kushirikiana na Tume ya ulinzi wa Taarifa Binafsi ili kuimarisha viwango vya Usalama wa Taarifa.

Balozi Adadi alitoa wito huo jijini Arusha wakati wa Hafla ya Ufunguzi wa Mafunzo ya siku nne ya Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi kutoka Taasisi zilizo chini ya chama cha mabenki Tanzania - TBA na chama cha watoa huduma za Mitandao ya simu Tanzania - TAMNOA ambapo alisema ushirikiano huo utajenga mazingira salama kwa Taarifa Binafsi za watu nchini.

"Napenda pia kutoa wito kwa sekta zote husika kushirikiana kwa karibu na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ili kuhakikisha kwamba viwango vya usalama wa taarifa vinazingatiwa na kwamba tunajenga mazingira salama kwa taarifa za watu". Alisema Balozi Adadi

Balozi Adadi alihitimisha risala yake ya Ufunguzi kwa kuwataka maafisa hao kuzingatia mafunzo hayo yanayotolewa na wabobezi kwenye kada ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

"Ninapenda kuchukua fursa hii kuwahimiza nyote mnaoshiriki mafunzo haya kuzingatia kwa makini kila somo mtakalofundishwa na watoa mada wetu ambao wote nimeona ni wabobezi wa masuala ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi. Usalama wa taarifa za watu ni jukumu letu sote, na ni muhimu kufanya kazi kwa bidii na uadilifu ili kuhakikisha kwamba tunatekeleza majukumu yetu ipasavyo". Alisema Balozi Adadi



Balozi Adadi Mohamed Rajabu, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi

# PDPC YATAKIWA KUTOA ELIMU ZAIDI KUHUSU ELIMU YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI.

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) imeagizwa kuimarisha elimu kuhusu dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi ili kuwasaidia Watanzania na taasisi mbalimbali kuelewa na kutekeleza Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kama alivyoagiza Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa uzinduzi wa tume hiyo.



Baadhi ya Viongozi wa PDPC, wakiwa kwenye picha ya pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhandisi Zena Ahmed Said (Aliekaa katikati) walipotembelea Ofisini kwake Agosti 20,2024

Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhandisi. Zena Ahmed Said, alitoa maelekezo haya wakati akizungumza na viongozi wa PDPC waliofika Zanzibar kwa lengo la kumtambulisha Mkurugenzi wa PDPC Ofisi ya Zanzibar. Pia ameipongeza Tume hiyo kwa mafanikio yaliyoonekana katika kipindi kifupi tangu kuanzishwa kwake.

"Inabidi jamii ijue umuhimu wa ulinzi wa taarifa binafsi, ambao sio tu unahusisha masuala ya Muungano bali pia unasimamia faragha za kila Mtanzania," alisema Mhandisi Zena

Pia alisisitiza kuwa ni muhimu kutoa elimu kwa jamii ili kila mtu ajue wajibu wake katika kutekeleza Sheria hii.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa ushirikiano wa karibu na wadau ili Tume iweze kufanyia kazi maelekezo ya Rais.

Mapema asubuhi, ujumbe huo ulijitambulisha kwa Dkt. Mngereza Mzee Miraji, ambae ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, nae ameihakikishia Tume ushirikiano na kuipongeza kwa kazi nzuri inayofanya.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa PDPC, Dkt. Emmanuel Mkilia, alisema PDPC imejipanga kutekeleza maelekezo ya Rais na tayari jitihada zinaendelea kupitia Mfumo wa Jamii X - change, ambao unalenga kuunganisha mifumo ya taasisi zote za umma na binafsi, unatarajiwa kuanza rasmi mwezi Oktoba, 2024. Taasisi zote zitapaswa kujiunga na kujisajili ili kushiriki katika kubadilishana taarifa.

Mkilia alifafanua kuwa mfumo huo wa kitaifa wa kubadilishana taarifa uliobuniwa na vijana wa Kitanzania, unalenga kuimarisha usalama, uharaka, na kulinda Taarifa Binafsi.







Dkt. Emmanuel Mkilia, Mkurugenzi Mkuu PDPC Akizungumza kwenye Kikao kazi cha Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma nchini, kilichoandaliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina na kili funguliwa Agosti 28, 2024 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

## ELIMU YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI YAWAFIKIA WENYEVITI WA BODI, WATENDAJI WAKUU WA MASHIRIKA NA TAASISI ZA UMMA

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Dkt. Emmanuel Lameck Mkilia Agosti 30,2024 amezungumzia dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi kwenye kikao kazi cha Wenyeviti wa Bodi na Watendaji Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma nchini, kilichofanyika Jijini Arusha katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa (AICC).

Akizungumza katika kikao kazi hicho Dkt. Mkilia alielezea Umuhimu wa Taasisi zote za Umma na Binafsi kujisajili na kupata cheti cha PDPC ili kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan wakati wa uzinduzi wa Tume kuhusu mifumo yote ya TEHAMA nchini kusomana ambapo amesema ili mifumo ya Taasisi moja na nyingine iweze kusomana namba ya cheti cha PDPC itatumika kuhakikisha Taarifa Binafsi za watu zinalindwa kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Na. 11, 2022.

Dkt. Mkilia pia alisema kuwa Taasisi au ofisi za umma na binafsi ambazo hazijajisajili PDPC zinapaswa kujisajili kabla au ifikapo tarehe 31 Disemba mwaka huu ili kutekeleza maagizo hayo ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Aidha Dkt. Mkilia ametumia jukwaa hilo kuwasilisha mpango kazi wa Tume kuhakikisha Mifumo itakayokuwa inasomana ili kurahisisha utoaji wa huduma nchini sambamba na kuhakikisha dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi inazingatiwa kuelekea Disemba 31, 2024 kama alivyoagiza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

# HABARI PICHA



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia akiwa na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Alice Mtulo alipomtembelea Ofisi kwakeJijini Dar es salaam na kuzungumza nae kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi hususani umuhimu wa kujisajili kwenye mfumo wa PDPC.




Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) Dkt. Emmanuel Lameck Mkilia amepokea tuzo mbili (2) kutoka Taasisi mbili tofauti, moja ni kutoka Chama cha Ukaguzi na Udhibiti wa Mifumo ya TEHAMA (ISACA) wakitambua mchango wake kama Mwanzilishi na Mkurugenzi Mkuu wa kwanza wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na nyingine kutoka kwenye Mkutano Mkuu wa Afrika kuhusu Ulinzi wa Taarifa na Faragha (Data Protection Africa Summit, 2024) ukitambua ushiriki wa PDPC kwenye Mkutano huo Mkubwa barani Afrika uliofanyika nchini Uganda kuanzia Desemba 02 – 06, 2024.






Baadhi ya washiriki wa mafunzo maalum ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa Mahakimu wakazi wafawidhi nchini wakiwa kwenye picha ya pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia (aliekaa Upande wa Kushoto). Mafunzo haya yalifanyika tarehe 13/11/2024 jijini Dar es Salaam




Oktoba 29, 2024, Mkurugenzi Mkaazi wa Minara Tanzania, Bw. Tudor Samuila akiwa na Mkuu wa Mahusiano ya Serikalini na Msimamizi wa Udhibiti wa Minara Tanzania - Bi. Dangie Kaniki wametembelea ofisi za Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) zilizopo Njedengwa – Dodoma kwa lengo la kuona namna Taasisi hiyo inavyoweza kushirikiana na PDPC katika masuala mbalimbali ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Nchini.



Bi. Shinuna Rashid (kushoto), Mkuu wa kitengocha Tehama Innerworks Consultants Legal and Business Services, Novemba 12, 2024 ametembelea Ofisi za Tumeya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) - Zanzibar na kufanya mazungumzo na Bi. Rehema Abdulah - Mkurugenzi wa PDPC Ofisi ya Zanzibar kwa lengo la kufahamu taratibu za kujisajili ili kutekeleza matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Namba 11 ya mwaka 2022.



BODI YA TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI YATEMBELEA MIFUMO YA USAJILI NA MALALAMIKO PDPC



Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia ametunukiwa Shahada ya Udaktari wa Falsafa yaani Doctor of Philosophy (PhD) ya Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi Desemba 12, 2024 na Mhe. Anne Makinda, Mkuu wa Chuo cha Ushirika Moshi (MoCU) ambapo alifanikiwa kufanya na kutetea utafiti juu ya Hatari za Usalama wa Mtandao na Matumizi ya Huduma za Kibenki Mtandaoni Nchini Tanzania.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hilton Law Group, Adv. Suzan Nelima akiwa na maafisa wengine wa Taasisi hiyo wametembelea Ofisi ya Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) zilizopo Njedengwa Dodoma September 12, 2024 kwa lengo la kuona namna Taasisi hiyo inavyoweza kushirikiana na PDPC katika masuala mbalimbali ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Nchini.






Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini (PDPC) ilishiriki warsha muhimu ya wadau wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuhusu maendeleo ya Mfumo wa Sera ya Usimamizi wa Taarifa iliyofanyika jijini Dar es Salaam Agosti 29 - 30, 2024. PDPC iliwakilishwa na Mkurugenzi wa Tafiti na Teknolojia, Dkt. Noe E. Nnko na Mwanasheria Mwandamizi,Bw. Godfrey Assenga, ambao walitoa maelezo kuhusu jinsi Mfumo wa Jamii X - change utakavyosaidia katika usimamizi wa Taarifa Kusomana na jinsi Jamii Portal itakavyowasaidia wananchi kufahamu matumizi ya taarifa zao binafsi.





Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Bw. Emmanuel Mkilia tarehe 23 Agosti 2024, ametembelea na kuwafundisha Wakufunzi na baadhi ya Wanafunzi Shule kuu ya Polisi Tanzania iliyopo Moshi mkoani Kilimanjaro pamoja na kuwapa elimu kuhusu dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi na kazi za Polisi, Teknolojia zinazoibukia, kuwajulisha maelekezo ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhusu elimu kwa Umma, Taasisi za Umma na Binafsi kujisajili PDPC, Mifumo ya TEHAMA kusomana na mapitio ya Sheria zinazohusu Mifumo hiyo kusomana.














# TAARIFA BINAFSI NI NYENZO MUHIMU KWENYE UCHUMI WA KIDIJITALI



Ulinzi wa Taarifa Binafsi ni miongoni mwa nyenzo muhimu za kufikia uchumi wa Kidijitali.

Hayo yalielezwa Jijini Arusha na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia wakati wa hafla ya Ufunguzi wa Mafunzo ya siku nne kwa Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi kutoka Taasisi zilizo chini ya chama cha mabenki Tanzania (TBA) na chama cha mabenki Tanzania - TBA na chama cha watoa huduma za Mitandao ya simu Tanzania - TAMNOA ambapo amesema maendeleo ya haraka ya kidijitali yameonyesha umuhimu mkubwa wa kulinda taarifa binafsi, kuzuia matumizi mabaya ya taarifa na uvujaji wa taarifa binafsi.

"Dunia yetu leo inaendeshwa na taarifa mbalimbali, huku taarifa binafsi zikiwa ni nyenzo muhimu katika biashara na na mwingiliano miongoni mwa watu" Alisema Dkt. Mkilia

Aidha Bw. Mkilia akaweka bayana umuhimu wa mafunzo hayo kwa maafisa wa ulinzi wa taarifa binafsi nchini. "Ikizingatiwa Tanzania iko katika jitihada za kuimarisha uchumi wa kidijitali, kundi hili ni muhimu sana katika kuujenga na kuimarisha uchumi wetu kwa kuhakikisha kuwa faragha na taarifa binafsi zinalindwa kwa mujibu wa Sheria yetu ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Na. 11 ya mwaka 2022 pamoja na Kanuni zake mbili, kanuni za Usajili na zile za kushughulikia malalamiko ya ukiukwaji wa sheria husika" alisema Dkt. Mkilia

Haya ni mafunzo ya kwanza kwa Maofisa wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi (DPO's) yaliyoandaliwa na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi PDPC kwa kushirikiana na Chama cha Mabenki Tanzania - TBA na Chama cha watoa huduma za Mitandao ya - TAMNOA.








# PDPC YAKUTANA NA MENEJIMENTI YA BODI YA MIKOPO (HESLB)

Viongozi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) wamekutana na Menejimenti ya Bodi ya Mikopo (HESLB), tarehe 19 Agosti, 2024 jijini DODOMA na kuwapatia Elimu kuhusu Dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi pamoja na wajibu wa wakusanyaji na wachakataji wa Taarifa Binafsi.

Viongozi hao ni Dkt. Noe Elisa, Kaimu Mkurugenzi wa Tafiti na Teknolojia za Ulinzi wa Taarifa Binafsi - PDPC na wakili Humphrey Mtuy, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria - PDPC ambapo walitumia jukwaa hilo kuzikumbusha Taasisi zote zinazokusanya na kuchakata Taarifa nchini kuhakikisha wanajisajili PDPC na kupata vyeti kabla ya Tarehe 31 Disemba, 2024 kama ilivyoagizwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan , Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa Uzinduzi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi tarehe 3 Aprili 2024.

Aidha kwa mujibu wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Na. 11 ya Mwaka 2022 Kifungu cha 14 (1) na cha (2) kila Taasisi inayokusanya na kuchakata Taarifa nchini inapaswa kusajiliwa na Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

# DIGITAL TANZANIA NI JAMBO ENDELEVU, SERIKALI ITALINDA FARAGHA ZA WATU




Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Bw. Mohammed Khamis Abdulla amewatoa hofu watanzania kuhusu Ulinzi wa Taarifa zao Binafsi tunapoelekea kwenye uchumi wa kidijitali.

Bw. Abdullah alibainisha hayo Agosti 27, 2024 jijini Arusha wakati wa kikao cha kufanya tathimini ya mradi wa Tanzania ya Kidigitali (DTP) kwa nusu muhula ambapo alisema Tanzania ya Kidigitali ni jambo endelevu hivyo Serikali italinda Faragha za watu kupitia Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC).

Uchumi wa kidigitali unahusisha mifumo kusomana ambapo mifumo hiyo itaweza Taasisi moja kubadilishana taarifa na taasisi nyingine kwa kuzingatia usalama, uharaka na ulinzi wa taarifa binafsi ambapo mabadilishano hayo ya taarifa yatahitaji ridhaa ya Muhusika wa taarifa.




Bw. Daniel Sarungi, Mkuu wa kitengo cha Uzingatiaji - PDPC akitoa mada kwenye kongamano la Anuai za kitaaluma lililofanyika jijini Arusha kwa Ushirikiano baina ya TLS kwa kushirikiana na TPAA

## TUENDANE NA KASI YA MABADILIKO YA TEKNOLOJIA YANAYOCHAGIZWA NA UJIO WA DHANA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

Dhana ya Ulinzi wa Taarifa imeleta mabadiliko makubwa ya teknolojia nchini, ikiwemo namna mifumo ya TEHAMA inavyoweza kubadilishana taarifa kwa kuzingatia misingi ya ulinzi wa taarifa binafsi pamoja na kumpa mwananchi ridhaa ya kuamua matumizi ya taarifa zake. Wanasheria nchini wamepitishwa kwenye mabadiliko hayo chanya na kuaswa kuanza kutumia mifumo ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu yao.

Wito huo ulitolewa jijini Arusha, Novemba 15, 2024 na Bw. Daniel Sarungi, Mkuu wa kitengo cha Uzingatiaji (Compliance) - Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) wakati akitoa mada kwenye kongamano la Anuai za kitaaluma lililoandaliwa na Chama cha Wanasheria Tanganyika kwa kushirikiana na Jumuiya ya Faragha Tanzania ambapo alisema Maafisa Ulinzi wa Taarifa wanapaswa kushiriki kwenye shughuli zote za Kuboresha au kujenga mifumo ya Taasisi ili kuimarisha Ulinzi wa Taarifa binafsi.

"Mifumo yote inayojengwa kwenye Taasisi Afisa Ulinzi (DPO) unatakiwa kuzingatia dhana ya faragha (Privacy by Design) kuanzia mifumo inaposanifiwa hadi inapojengwa na kutumika, hii itakusaidia kusimamia utekelezaji wa Sheria ya ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa ufanisi" , alisema Bw. Sarungi

Aidha Bw.Sarungi aliweka bayana kwamba Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi imekuja kuhakikisha Ulinzi wa faragha unazingatiwa sambamba na kuwezesha Uchumi wa Kidigitali nchini. "Lengo la Tume ni Kuwezesha Uchumi wa Kidigitali, kwa kumpatia mwananchi mamlaka kamili ya kutumia taarifa zake kwa usalama bila kuathiri faragha yake."

Pia aliwasisitiza wanasheria nchini waanze kuangazia swala la udhibitishaji wa nyaraka laini yaani e-Notary, Digital Signature pamoja na kuweka mpango wa kufanya mapitio ya utaratibu wa utendaji (Business Process Reengineering) ili kuweza kumudu soko linalokuja na mabadiliko ya Teknolojia.



## PDPC YATOA MAFUNZO YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI KWA CRDB

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) imetoa mafunzo ya siku moja kwa watumishi wa CRDB kuhusu ulinzi wa taarifa binafsi na namna ya kutekeleza sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi katika shughuli zao za kila siku.

Akitoa utangulizi wa mafunzo hayo yaliyofanyika katika ukumbi wa hoteli ya Coral Beach jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Utafiti na Uzingatiaji PDPC Mhandisi Stephen Wangwe ameeleza kuwa, majukumu ya PDPC ni kusimamia utekelezaji wa sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa kuwatambua na kuwasajili wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi ili kuhakikisha ulinzi wa taarifa walizonazo unazingatiwa.

"Tupo kwa ajili ya kulinda faragha za watu katika utekelezaji wa shughuli za kila siku zinazohusisha matumizi ya taarifa zao binafsi. Hii sheria haiji kukinzana na sheria nyingine ila inazingatia misingi yote nane ya ulinzi wa taarifa binafsi ili kuhakikisha muhusika wa taarifa anakuwa salama wakati wa matumizi ya taarifa zake. Ndiyo maana taasisi zote za umma na binafsi nchini ni lazima zihakikishe kwenye utekelezaji wa majukumu yake taarifa binafsi zinalindwa."

"Tunaanza kuwasajili na kuwapa uelewa taasisi zinazokusanya na kuchakata taarifa nchini ili zizingatie ulinzi wa taarifa binafsi na muhusika wa taarifa hizo awe na uhakika kuwa taarifa zake zinatumika vizuri" amesema Mhandisi Stephen Wangwe.

Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi inasapoti uchumi wa kidijitali kwa kulinda haki ya faragha kwa kumpa nafasi muhusika wa taarifa kukubali au kukataa taarifa zake kutumika na kuongeza uaminifu wa wateja kwa watoa huduma wao.

Utoaji wa mafunzo hayo ni moja ya njia ya PDPC kuwashirikisha wadau wao na kuwapa uelewa juu ya dhana ya ulinzi wa taarifa binafsi ili kuhakikisha dhana hiyo inaeleweka na utekelezaji wa sheria ya ulinzi wa taarifa binafsi unafanikiwa.

## ZINGATIENI HAKI YA FARAGHA, MNAPOSANIFU MIFUMO YA TEHAMA

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Dkt. Emmanuel Mkilia amezitaka Taasisi zote nchini kuhakikisha zinazingatia haki ya Faragha kuanzia wanapo sanifu hadi wanapojenga mifumo ya TEHAMA inayohusisha Taarifa Binafsi kwenye Taasisi zao.

Dkt. Mkilia alitoa maagizo hayo tarehe 22 Agosti, 2024 jijini Dodoma wakati akifunga Semina ya siku mbili ya kuandaa Muongozo wa Usimamizi na Ulinzi wa Taarifa ambapo alisema ni muhimu kulinda Taarifa Binafsi na kujali faragha za watu tangu mifumo ya Tehama inapoanza kusanifiwa hadi inapojengwa.

Wakati huo huo Dkt. Mkilia akazikumbusha Taasisi hizo kuhakikisha wanajisajili na kupata vyeti vya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kutoka Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) kabla ya Disemba 31,2024.

TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI



## WASILIANA NASI

Huduma kwa wateja:
0718462536, | 0736110505, | 0744057652
*Baruapepe: helpdesk@pdpc.go.tz*

Au tufuatilie kwenye mitandao ya kijamii;

@pdpc.tz @pdpc_tz www.pdpc.go.tz

Pia unaweza kujiunga na Chaneli yetu ya WhatsApp kwa jina la Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC)

www. pdpc.go.tz

*"Faragha yako ni Wajibu Wetu"*

## ASANTENI WASHIRIKA

**LIMETOLEWA NA:**
**Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**
**Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC)**
**S.L.P 1105, Jengo la UCSAF Dodoma**